Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

HEKIMA NI UHURU

HEET
HIGHER EDUCATION FOR ECONOMIC TRANSFORMATION

Toleo la
07

# Jarida la HEET UDSM

*Toleo la Machi 2025*




HEET
Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi

## Ndani ya Toleo hili...




**Teknolojia za Dijitali**
Kuboresha Mfumo wa Ufundishaji na Ujifunzaji UDSM
Uk. 7



**UDSM kuwa**
Kituo Mahiri katika Utafiti wa Sayansi ya Bahari Afrika **- JK**
Uk. 9



**Mabadiliko makubwa**
katika Miundombinu ya TEHAMA na Teknolojia Maizi UDSM
Uk. 22

# YALIYOMO

| | |
|---|---|
| 3 | Salamu za Makamu Mkuu wa Chuo |
| 4 | Ujumbe wa Mratibu |
| 5 | Uunganishaji wa Vifaa vya Studio za Kisasa za Maltimedia Waendelea kwa Ufanisi UDSM |
| 6 | Mfumo wa Akaunti Moja na Uboreshaji wa Baruapepe kufanikisha Kampasi Maizi UDSM |
| 7 | Teknolojia za Dijitali Kuboresha Mfumo wa Ufundishaji na Ujifunzaji UDSM |
| 9 | Kikwete: UDSM kuwa Kituo Mahiri katika Utafiti wa Sayansi ya Bahari Barani Afrika |
| 10 | Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi, UDSM wajadili maeneo muhimu ya ushirikiano |
| 11 | Rais Mwinyi Abainisha Wajibu wa IMS-UDSM katika Utekelezaji wa Sera ya Uchumi wa Bluu |
| 13 | Ujumbe wa Naibu Mratibu |
| 14 | Tahariri |
| 15 | Picha za Matukio |
| 17 | Sera ya Ujifunzaji Mtandaoni UDSM Yazinduliwa |
| 18 | Kampasi Maizi yaanza UDSM kwa Uunganishaji na Usambazaji wa Mkongo wa Mtandao |
| 19 | Teknolojia ya Kisasa Kuifanya UDSM Kinara katika Mabadiliko ya Dijitali ya Elimu ya Juu |
| 20 | Waziri Jafo asisitiza ubiasharishaji wa matokeo ya utafiti na kuzingatia ustawi wa jamii |
| 21 | Benki ya Dunia yatoa wito wa kuharakisha utekelezaji wa shughuli za Mradi wa HEET huku UDSM ikionyesha maendeleo ya kupigiwa mfano |
| 22 | Mabadiliko makubwa katika Miundombinu ya TEHAMA na Teknolojia Maizi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) |

# Salamu za Makamu Mkuu wa Chuo



**Prof. William A. L. Anangisye**

## Makamu Mkuu wa Chuo

Kwa niaba ya uongozi wa UDSM, nina furaha kuwakaribisha wasomaji wetu kwenye Toleo la Saba la Jarida la HEET-UDSM, ambapo tunaendelea kutekeleza kwa vitendo dhamira yetu ya kuwapa wadau wetu taarifa kuhusu maendeleo ya mradi huu wa kimkakati.

Jarida hili linatumika kama chombo cha kuwapa wadau taarifa za utekelezaji wa Mradi wa HEET na kupokea mrejesho ili kuboresha utekelezaji wake. Ufuatiliaji na utoaji wa taarifa kuhusu utekelezaji wa mradi ni muhimu kwa kuwa ni sehemu ya mpangomkakati wa Chuo wa kuchangia vipaumbele vya maendeleo ya taifa.

Chuo kimeendelea kuufuatilia na kuutathmini mradi huu kwa umakini ili kuhakikisha kwamba kunakuwa na mafanikio katika kuyafikia malengo yake ya maendeleo. Tangu toleo lililopita, UDSM imechukua hatua kadhaa za kimkakati ambazo zimeleta maendeleo makubwa kuelekea kuyafanikisha malengo haya.

Maendeleo ya ujenzi katika maeneo kumi na moja yamevuka asilimia 50%, huku mitaala yote iliyoboreshwa ikiwa imeidhinishwa na Seneti kwa ajili ya kuendelea na hatua ya ithibati kutoka katika Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania. Lengo letu ni kuendelea kuhakikisha shughuli za ujenzi zinakamilika kwa wakati. Kwa upande wa mitaala, tunatarajia mchakato wa kupata ithibati utakuwa umekamilika katika mwaka ujao wa masomo (2025/2026).

Hatua muhimu ilikuwa uwekaji rasmi wa jiwe la msingi kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Taaluma na Utawala katika Taasisi ya Sayansi za Bahari (IMS) huko Buyu-Zanzibar, tarehe 5 Januari, 2025.

Sherehe za uwekaji wa jiwe la msingi kwa kampasi za Kagera na Lindi zimepangwa kufanyika mnamo Aprili na Mei 2025, mtawalia.

Ili kuwezesha uanzishaji wa kampasi za Kagera na Lindi, UDSM inaandaa mpango wa uendeshaji na uanzishaji unaoendana na mfumo wake endelevu. Mpango huu unatoa kipaumbele katika uthibitishaji wa kampasi, utoaji wa programu za masomo pamoja na upatikanaji wa rasilimali watu, fedha na miundombinu. Vilevile, tunawakaribisha watu wa jamii jirani na wadau wa maendeleo kuchunguza fursa zitakazotokana na kampasi hizi mpya.

Kwa mara nyingine, ninakukaribisheni wasomaji wetu na ninatumaini kuwa toleo hili litakuwa na manufaa kwetu sote.

# Ujumbe wa Mratibu



## Prof. Bernadeta Killian

### Mratibu wa HEET-UDSM

Toleo hili linatoa fursa nyingine ya kutafakari maendeleo yaliyofikiwa katika utekelezaji wa Mradi wa HEET katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Tangu taarifa yetu ya mwisho, Chuo kimepiga hatua muhimu katika nyanja mbalimbali za mradi huu.

Maendeleo ya ujenzi katika maeneo sita yaliyotengwa jijini Dar es Salaam, Zanzibar, Lindi na Kagera yamefikia takribani asilimia 50 ya kukamilika. Tukio muhimu lilikuwa uwekaji wa jiwe la msingi katika jengo la utawala na shughuli za kitaaluma katika Taasisi ya Sayansi za Bahari Zanzibar, lililowekwa rasmi na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, tarehe 5 Januari, 2025. Mipango inaendelea kwa ajili ya hafla kama hiyo katika kampasi za Kagera na Lindi kwa miezi ijayo.

Katika kuboresha mitaala na kuzingatia suala la ubunifu katika ufundishaji mbali na mambo mengine,, Seneti ya Chuo imepitisha mitaala 215 (92 kutoka katika fani za kipaumbele na 123 kutoka katika fani zingine) kwa ajili ya kupatiwa ithibati na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania. Lengo letu ni kukamilisha mchakato huu kabla ya mwaka wa masomo wa 2025/2026.

Katika kukuza shughuli za utafiti na ubunifu, UDSM inaandaa tukio ambapo watafiti na wabunifu wataonesha kazi zao kwa wawekezaji ili kuleta mvuto wa kibiashara. Tukio hili linatarajiwa kufanyika mwishoni mwa mwezi Machi, 2025.

Kuhusu uhusiano wa tasnia, Kamati za Ushauri wa Tasnia (IACs) zinaendelea kufanya mikutano ya mara kwa mara kama ilivyopangwa, huku mikataba ya maridhiano 18 kati ya 25 ikiwa imesainiwa kati ya UDSM na kampuni mbalimbali. Vilevile, wanataaluma na wafanyakazi wa kiufundi 35 wameshiriki katika kazi za tasnia mbalimbali ili kuimarisha ushiriki wa wanajumuiya katika kazi hizi kwa vitendo.

Katika kukuza mabadiliko ya kidijiti, jitihada kadhaa zimekamilika, huku zingine zikiendelea. Kufikia Februari, 2025, asilimia 70 ya mipango ya TEHAMA chini ya Mpango wa Kimkakati wa Utekelezaji wa Mradi wa HEET-UDSM ilikuwa imekamilika. Mafanikio muhimu ni pamoja na uunganishaji wa mtandao mpya wa data wa TEHAMA, maboresho ya mifumo ya ufundishaji na ujifunzaji na uboreshaji wa majukwaa kama *Moodle LMS, Massive Open Online Courses na Open Education Resources (OER).*

Mafanikio mengine ni pamoja na ununuzi wa vifaa na programu za watu wenye mahitaji maalumu, uundaji wa Mfumo wa Jarida la Mtandaoni (OJS), Mfumo wa Usimamizi wa Miradi (PMS) na Mfumo wa Usajili Jumuishi (SSO) ili kurahisisha utumiaji wa majukwaa ya kidijiti UDSM.

Uunganishaji wa akiliunde na teknolojia ya mfumo wa taarifa za kijiografia (GIS) pia umeimarisha uchambuzi wa matumizi ya ardhi kwa watafiti. Vilevile, studio mpya za maltimedia katika Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia (CoET) sasa zinasaidia uandaaji wa maudhui ya kidijiti na ujifunzaji wa masafa.

Chuo pia kinaendelea kufuatilia maendeleo ya wanataaluma wake, ambapo mfanyakazi mwingine amehitimu programu ya umahiri nchini Uingereza, na hivyo kuongezeka kwa idadi ya wafanyakazi wanane waliorejea UDSM ili kufanikisha dhamira ya Chuo.

Ufuatiliaji wa utekelezaji wa shughuli za mradi unaendelea kuwa kipaumbele chetu. Zipo zana na mifumo mbalimbali inayohakikisha utekelezaji wa mradi unafanyika kwa ufanisi. Licha ya changamoto zilizopo, utekelezaji unaendelea vizuri na UDSM imejizatiti katika kuendeleza mpango wake endelevu ili kukabiliana na mahitaji yanayojitokeza.

Maendeleo haya yamewezekana kupitia msaada mkubwa kutoka kwa wadau wetu ambao tunawahimiza kuendelea kushirikiana nasi ili kuhakikisha kunakuwa na mafanikio katika Mradi wa HEET.

# Uunganishaji wa Vifaa vya Studio za Kisasa za Maltimedia Waendelea kwa Ufanisi UDSM

*Na Dotto Kuhenga, HEET-UDSM*



Katika hatua muhimu ya kuboresha ujifunzaji wa kidijitali na maendeleo ya teknolojia, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kimeanzisha studio za kisasa za maltimedia katika ndaki zake mbili zinazohusika na Uhandisi, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Studio hizi zinazofadhiliwa na Mradi wa HEET, zinalenga kuleta mapinduzi katika mbinu za ujifunzaji kwa njia ya mtandao na njia mseto, pamoja na mapinduzi katika mazingira ya kisasa ya elimu ya juu.

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Taaluma, Prof. Bonaventure Rutinwa, alisisitiza umuhimu wa studio hizi, akirejelea mahitaji ya soko la kimataifa na mageuzi ya kasi ya teknolojia katika elimu ya juu.

"Studio hizi za kisasa zinaendana na Dira ya UDSM ya 2061 ya kuwa kituo kinachoongoza kwa ubora katika ufundishaji, utafiti na utoaji wa huduma kwa jamii. Studio hizi zitaimarisha uzoefu katika ujifunzaji na kutoa fursa za kisasa za ujifunzaji wa mtandaoni," alisema Prof. Rutinwa.

Kwa mujibu wa Mtaalamu wa Elimu na Teknolojia ya dijitali wa Mradi wa HEET-UDSM, Dkt. Kwame Ibwe, studio za maltimedia zimeanzishwa katika Ndaki ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (CoICT) na Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia (CoET).

"Uunganishaji wa vifaa vya studio hizi za maltimedia umekaribia kukamilika. Tunasubiri uunganishaji wa vifaa CoET, huku ukarabati na uwekaji wa teknolojia ya kisasa katika studio ya CoICT ukiendelea vyema," alisema Dkt. Ibwe.

### *Mazingira Changamani na Shirikishi ya Kujifunzia*

Alibainisha kuwa studio hizo zitaweka mazingira changamani na shirikishi ya kujifunza, huku zikiwawezesha wanafunzi kupata ujuzi muhimu wa kidijitali unaohitajika katika soko la sasa la ajira.

"Kwa kupata zana za kisasa za uandaaji wa sauti na picha, wanafunzi watakuwa na uwezo wa kuandaa maudhui ya kielimu ya ubora wa juu, kufanya majaribio ya mtandaoni na kushiriki katika mijadala ya masomo, hivyo kukuza uelewa wao wa dhana changamani za uhandisi na TEHAMA," alisema Dkt. Ibwe.

Aidha, alisisitiza kwamba studio hizi zitawawezesha kuwa na ufundishaji na ujifunzaji unaoendana na mabadiliko na teknolojia. Wahadhiri watakuwa na uwezo wa kurekodi, kuhariri na kupakia mihadhara, hivyo, kufanya nyaraka hizo kupatikana kwa wanafunzi kwa urahisi popote pale walipo.

"Maendeleo haya yataongeza ufanisi wa programu za ujifunzaji wa mtandaoni na za ujifunzaji mseto/changamani huku zikihakikisha kwamba elimu katika UDSM inabaki kuwa ya ubunifu na inayoweza kubadilika kulingana na mabadiliko ya kiteknolojia," aliongeza.

Kwa upande mwingine, Mkurugenzi wa Kurugenzi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) wa UDSM, Dkt. Salome Maro, alisisitiza umuhimu wa studio hizi za maltimedia katika kukuza ushirikiano kati ya wanafunzi, walimu na wataalamu katika tasnia kupitia zana za kisasa za mikutano ya mtandaoni na mawasiliano ya dijitali.

"UDSM itakuwa na uwezo wa kuandaa semina, warsha na mihadhara ya mtandaoni kwa kushirikiana na wataalamu kutoka maeneo mbalimbali duniani kote. Jambo hili litatengeneza mazingira ya kimataifa ya kujifunzia ambapo wanafunzi wataweza kupata ufahamu kuhusu mbinu bora za kitasnia na mabadiliko yanayotokea katika uhandisi na TEHAMA," alisema Dkt. Maro.






***Usimikaji wa projekta imara zenye mfumo wa Android kupitia Mradi wa HEET — kuboresha ujifunzaji shirikishi na matumizi ya multimedia katika kumbi za mihadhara***

# Mfumo wa Akaunti Moja na Uboreshaji wa Baruapepe kufanikisha Kampasi Maizi UDSM

*Na Remmy Wilson, HEET-UDSM*




***Uzinduzi wa ukurasa wa kuingia wa Mfumo wa SSO wa UDSM — kurahisisha upatikanaji wa mifumo yote ya taasisi kwa kutumia nywila moja salama kwa watumishi na wanafunzi***

Kama sehemu ya mpango wake wa kuwa na kampasi maizi, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimetekeleza mpango wa kuwa na mfumo wa pamoja wa kimtandao na mpango wa kimapinduzi utakaowawezesha wanajumuiya kupata huduma zote za chuo kwa kutumia seti moja ya taarifa.

Mpango huu unaotekelezwa chini ya Mradi wa HEET, ni hatua muhimu kuelekea kuongeza usalama na ufanisi wa kiutendaji, kupunguza vihatarishi vya kumiliki akaunti tofautitofauti na kuboresha michakato ya utendaji ya Chuo.

Dkt. Kwame Ibwe, Mtaalamu wa Elimu na Mfumo wa Dijitali wa HEET-UDSM, alisema kuwa mpango huu unahitimisha safari ya muda mrefu ambapo wanajumuiya wake walilazimika kuwa na nywila nyingi kwa wakati mmoja. “Kwa kutumia mfumo huu, nywila moja inatosha kufungua mifumo yote, iwe ni kuingia kwenye baruapepe, kanzidata za utafiti au Mfumo wa Usimamizi wa Ujifunzaji (LMS).”

Dkt. Ibwe alikumbusha kuwa kwa miaka mingi, wafanyakazi na wanafunzi wa UDSM walikuwa wakiingia kwenye mifumo mbalimbali kwa kutumia majina na nywila tofauti. mathalani, katika kuingia kwenye baruapepe, Mfumo wa Usimamizi wa Ujifunzaji na mifumo ya utawala. “Hii haikuwa tu usumbufu kwa watumiaji bali pia ilikuwa ni kikwazo cha ufanisi.”

“Usahaulifu wa nywila, makosa ya mara kwa mara ya kuingia na mchakato mrefu wa kurekebisha nywila ilikuwa sehemu ya maisha ya chuo kikuu. Sasa, enzi mpya ya urahisi wa kidijiti inadhihirika UDSM, enzi inayofanya usumbufu kuwa historia,” alisema Dkt. Ibwe akiwa na matumaini makubwa ya kufanikiwa.

### *Mabadiliko makubwa katika Mfumo wa Baruapepe*

Dkt. Ibwe alielezea zaidi kwamba katika mchakato huu wa mabadiliko ya kidijiti, pamoja na mfumo jumuishi wa mawasiliano, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pia kinafanya uboreshaji mkubwa wa mfumo wake wa baruapepe. Hapo awali, nafasi ndogo kwa ajili ya hifadhi katika baruapepe iliwalazimu watumiaji kufuta baruapepe mara kwa mara ili kuwa ndani ya ukomo wa MB 500.

“Mawasiliano muhimu ya utafiti, ushirikiano na utawala yalikuwa katika hatari ya kupotea. Sasa, kwa mfumo mpya, kila mtumiaji atapata hifadhi ya GB 5 ili kuhakikisha kuwa baruapepe, viambatisho na nyaraka muhimu zinapatikana kila wakati zinapohitajika,” aliongeza Dkt. Ibwe.

Alisema kwamba uboreshaji huu wa baruapepe pia utaleta muunganiko wa moja kwa moja na zana za ushirikiano za kisasa. “Fikiria mhadhiri anayeandaa mtihani mtandaoni katika LMS, kusambaza nyaraka kupitia Microsoft 365 au Google Drive kwa urahisi huku wanafunzi wakishirikiana kufanya mazoezi. Yote haya yatafanyika katika mfumo mmoja ulioounganishwa.”

“Ufanisi wa aina hii si ndoto tena; unakuwa halisi ndani ya UDSM. Pia, hatua za usalama zilizoboreshwa, ikiwamo uthibitisho wa vipengele vingi (MFA) na vichambuzi vyenye nguvu vya spam, utahakikisha ulinzi wa mawasiliano nyeti ya chuo kikuu dhidi ya vitisho vya kimtandao,” alisema Dkt. Ibwe.

Alisisitiza kwamba utekelezaji wa mpango wa mfumo jumuishi wa kimtandao na uboreshaji wa mfumo wa baruapepe umekamilika kwa 95%, na athari za mabadiliko haya tayari zinaonekana. “Chuo kinakaribia kufikia malengo yake ya mabadiliko ya kidijiti, kuhakikisha ushirikiano na mawasiliano ya kimasomo na kiakademia.”

Aliendelea kueleza kwamba, dira ya kampasi maizi ya UDSM haikuwa tu kuboresha teknolojia, bali pia kutengeneza mazingira ambapo ujifunzaji, ufundishaji na utawala vinastawi.

Mpango huu unadhihirisha hatua muhimu katika kuibadilisha UDSM kuwa taasisi inayounganishwa kikamilifu kwa mfumo wa dijitali. Mustakabali wa elimu ya juu wa UDSM ni wa kisasa, usio na vikwazo na salama, na tayari umeanza kutekelezwa.

# Teknolojia za Dijitali Kuboresha Mfumo wa Ufundishaji na Ujifunzaji UDSM

*Na Jackson Isdory, HEET-UDSM*



*Uwekaji wa teknolojia za darasa mahiri, zikiwemo mimbari dijitali na vifaa vya kisasa—kubadilisha vyumba vya kawaida vya kufundishia kuwa mazingira ya kisasa ya ujifunzaji yenye teknolojia*

Kama sehemu ya kubadilisha mtindo wa ufundishaji na ujifunzaji ili kuendana na mtaala wa vitendo, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kimepiga hatua kubwa katika ajenda yake kuendana na maendeleo ya dijitali kwa kuanzisha teknolojia za darasa maizi.

Akizungumzia mpango huo, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo (Taaluma) wa UDSM, Prof. Bonaventure Rutinwa, alisema kuwa mpango huu wa kimkakati wa kuwekeza katika teknolojia za kisasa katika elimu unawiana na dhamira ya Chuo ya kutengeneza mazingira ya kujifunza yenye mwelekeo wa kidijiti huku yakiwa jumuishi na wezeshi kwa wanafunzi na wahadhiri.

"Hatua hii ya kimkakati inawiana na dira ya Chuo ya kuwa kituo bora kinachoongoza katika ufundishaji, utafiti na utoaji wa huduma kwa jamii. Teknolojia hizi zitaimarisha uzoefu wa kujifunza, kutoa fursa za kujifunza kwa urahisi na kuhakikisha elimu bora inapatikana kwa wote, wakiwamo wale watakaojifunza kwa masafa," amesema Naibu Makamu Mkuu wa Chuo.

Kwa mujibu wa Mtaalamu wa Elimu na Teknolojia ya Dijitali wa Mradi wa HEET-UDSM, Dkt. Kwame Ibwe, mchakato huu unaoratibiwa na Mradi wa HEET, utabadilisha kabisa uzoefu wa ufundishaji na ujifunzaji kwa kuanzisha zana za kisasa kama vile mbao maizi, mifumo ya kurekodi mihadhara na zana za ushirikishaji wa kidijiti.

"Zana nyingine za ubunifu ambazo zinaendelea kununuliwa ni pamoja na mifumo ya ujifunzaji inayoendeshwa na akiliunde na ushiriki wa mafunzo wa kimtandao ili kusaidia ufundishaji wa madarasa mengi kwa wakati mmoja na ufundishaji masafa wa masomo," alisema Dkt. Ibwe.

Vilevile, UDSM imekamilisha uwekaji wa vifaa vya kisasa vya maltimedia kwa ajili ya kumbi za mihadhara, zikiwamo projekta za Android zenye uwezo mkubwa, majukwaa ya dijitali na mifumo ya sauti ya kiwango cha juu.

"Maboresho haya yanatarajiwa kukuza ubora wa elimu na kupanua wigo wa ujifunzaji tofauti na mazingira jadia ya sasa ya kuwa na darasa la ana kwa ana," alisema.

### *Kupanua Wigo, Kuboresha Matokeo ya Ujifunzaji*

Teknolojia za darasa maizi na vifaa vya maltimedia vitarahisisha ujifunzaji mseto, ambapo zana za kidijiti zitajaziliza ufundishaji jadia wa ana kwa ana. Mifumo ya ujifunzaji inayoendeshwa na akiliunde na ushiriki wa darasa kimtandao utakuza ushirikiano na wataalamu wa kimataifa pamoja na taasisi mbalimbali.

Dkt. Ibwe alisema kwamba teknolojia hizi zitawapatia wanafunzi mtazamo wa kimataifa kuhusu masomo yao na hivyo kuzalisha wahitimu wenye ujuzi, maarifa na ushindani wa kimataifa ambao wanaweza kukidhi mahitaji ya soko la ajira yanayobadilika.

Mradi wa HEET uliojikita katika kuboresha miundombinu ya kidijiti unaendana na mageuzi makubwa ya elimu nchini Tanzania, yenye lengo la kuzalisha wahitimu wenye umahiri kwa ajili ya uchumi wa kidijiti. Pia, teknolojia mpya zitasaidia juhudi za utafiti za Chuo, kutoa utafiti unaoendeshwa na data na kukuza uvumbuzi," alisema Dkt. Ibwe.



Mimbari

### *Kuziba Pengo kati ya Ufundishaji na Teknolojia*

Mkutano wa Jumuiya ya Wanataaluma wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDASA) pia umepongeza mpango wa UDSM kuwekeza katika mfumo wa dijitali. Prof. John A.M. Mahugija, mfanyakzi kutoka Idara ya Kemia na Mwenyekiti wa UDASA, alisisitiza athari chanya zinazotarajiwa katika utoaji wa elimu.

"Uanzishaji wa teknolojia za darasa maizi kwa kiasi kikubwa utaimarisha mbinu zetu za ufundishaji. Wanazuoni sasa wanaweza kutengeneza mazingira shirikishi na ya kuvutia katika ujifunzaji ambayo yatakuwa na manufaa kwa walimu na wanafunzi," alisema Prof. Mahugija.

Aliendelea kueleza kwamba maendeleo hayo pia yataunga mkono utafiti na juhudi za ushirikiano, hususani katika kushirikiana na majukwaa ya kiakademia ya kimataifa. "Ninawaomba wenzangu wa UDASA kulinda vifaa hivi; na uongozi wa Chuo kuhakikisha uendelevu wake."

Chama cha Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (DARUSO) kimepokea mageuzi haya kwa furaha. Rais wa DARUSO, Bw. Tyson Lucas Kwigendaho, alielezea hatua hii kama 'mabadiliko makubwa' katika mchakato wa ujifunzaji kwa wanafunzi.

"Hatua hizi zitatupatia zana za kisasa na majukwaa ya kujifunza kwa kutangamana zaidi na ujifunzaji kwa njia ya masafa," alisema.

Aliongeza, "Pia, vifaa vipya vya maltimedia vitaboresha ubora wa uwasilishaji na mihadhara, na kufanya ujifunzaji kuwa wa kuvutia na wenye ufanisi. Hatua hii inaonyesha kwamba uongozi wa Chuo na serikali wanajizatiti katika kutoa uzoefu wa kutoa elimu inayoendana na mabadiliko yanayoendelea ulimwenguni."

Bi. Evaline Eliya Pallangyo, mwanafunzi wa mwaka wa tatu wa Shahada ya Sanaa ya Takwimu, aliupongeza uongozi wa Chuo kwa kutoa kipaumbele kwa mahitaji na matarajio ya kimasomo. Alisisitiza umuhimu wa kutunza vifaa hivyo vipya.

"Ninapongeza maendeleo haya, kwa kuwa dunia inakua kwa kasi, na karibu kila kitu kinaendeshwa na akiliunde. Hatupaswi kubaki nyuma. Vifaa hivi ni ghali, ninawashauri wanafunzi wenzangu na watumiaji wote kwa ujumla kuvitunza vizuri vifaa hivi. Pia, Chuo kinapaswa kutenga bajeti ya matengenezo ili kuhakikisha teknolojia hizi zinaendelea kutumika," alisema.

Wakati huohuo, Dkt. Salome Maro, Mkurugenzi wa TEHAMA wa UDSM, aliwahakikishia wadau na uongozi wa Chuo kuhusu uvumbuzi wa kielimu, akisisitizia mbinu ya kimkakati katika utekelezaji wa teknolojia hizi.

"Kipaumbele kimetolewa kwa kumbi za mihadhara na maabara katika vitengo mbalimbali. Uongozi wa Chuo umejizatiti kutoa mafunzo ya kutosha ili kuhakikisha kuwa wanafunzi na wafanyakazi wanaweza kutumia na kutunza mifumo hii ya kisasa kwa ufanisi," alisema Dkt. Maro.

Hatua hii ya ujasiri ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuelekea kutoa elimu inayoendeshwa kwa mfumo wa dijitali inaonyesha namna Chuo kilivyojizatiti bila kutetereka katika ubora wa ufundishaji, utafiti na huduma kwa umma, huku kikiwa mfano wa kuigwa katika taasisi za elimu ya juu ndani na nje ya nchi.




***Chumba cha uangalizi chenye vifaa vya kisasa vikiwemo skrini za ukutani kwa ajili ya ufuatiliaji wa moja kwa moja wa shughuli katika mtandao mkuu (kituo cha data) mpya kupitia Mradi wa HEET***

# Kikwete: UDSM kuwa Kituo Mahiri katika Utafiti wa Sayansi ya Bahari Barani Afrika

***Na Dotto Kuhenga, HEET-UDSM***



*Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete (wa pili kushoto-mstari wa mbele) akiwaongoza viongozi wengine kuelekea kwenye eneo la kuweka jiwe la msingi la jengo la taaluma na utawala katika Taasisi ya Sayansi za Bahari (IMS) ya UDSM, Buyu, Zanzibar linalojengwa kupitia Mradi wa HEET. Viongozi wengine kushoto kwa Mkuu wa Chuo ni pamoja na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Prof. Adolf Mkenda (Mb) na Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Mhe. Balozi Mwanaidi Maajar. Tukio hili lilifanyika tarehe 5 Januari, 2025*

Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, ameonesha kuridhishwa na maendeleo ya ujenzi wa majengo mapya katika Taasisi ya Sayansi za Bahari Zanzibar kupitia Mradi wa HEET.

Amesema kwamba mara baada ya ujenzi kukamilika, Chuo kinakusudia kuwa kituo mahiri cha utafiti wa sayansi ya bahari katika Ukanda wa Afrika.

Dkt. Kikwete alitoa kauli hiyo wakati wa ziara yake ya hivi karibuni katika Taasisi ya Sayansi za Bahari huko Buyu, Zanzibar, kwa ajili ya kutathmini maendeleo ya Mradi wa HEET.

Mradi huo ambao umegharimu takribani ShT. bilioni 11, unatarajiwa kuimarisha uwezo wa taasisi hiyo katika kufanya utafiti wa kisayansi kuhusu maisha ya baharini na mifumo ya ikolojia.

"Nimekuja kukagua ujenzi ili kuona tulipofikia. Mara ya mwisho nilipokuwa hapa, eneo hili lilikuwa na msingi tu ambao umekuwapo kwa miaka 20. Leo, nimefurahi na nimehamasika kuona maendeleo makubwa," alisema Dkt. Kikwete.

Ameongeza, "Kazi inafanyika kwa ufanisi, na kwa mujibu wa ahadi iliyotolewa, ujenzi utakamilika Agosti mwakani, mwezi mmoja kabla ya muda wa mkataba kumalizika."

### *Kituo Muhimu cha Masomo ya Baharini na Bioanuwai*

Akisisitiza umuhimu wa taasisi hiyo, Dkt. Kikwete alieleza kuwa dhamira ya mradi huu ni kuanzisha kituo mahiri cha utafiti wa sayansi ya bahari kwa ukanda huu.

"Sidhani kama kuna taasisi nyingine yenye ukubwa huu, na ninaamini kwamba mara tu tutakapokamilisha ujenzi huu, kukawa na maabara zenye vifaa vya kisasa, wahadhiri wenye sifa na watafiti wanaojituma, taasisi hii itakuwa kituo mahiri cha taaluma ya sayansi za bahari na bioanuwai," alisema.

Vilevile, Dkt. Kikwete aliishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, inayoongozwa na Dkt. Hussein Mwinyi, kwa kutoa kipaumbele katika mradi huu.

Alisisitiza kuwa miundombinu bora inayojengwa UDSM itachochea maendeleo ya kitaaluma na kiutafiti katika uwanja wa sayansi ya bahari.

Taasisi ya Sayansi za Bahari ya UDSM inatarajiwa kuvutia watafiti kutoka ndani na nje ya nchi, kukuza maendeleo ya maarifa katika taaluma ya sayansi za bahari na uhifadhi wa mazingira.

# Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi, UDSM wajadili maeneo muhimu ya ushirikiano

*Na Zamda George, HEET-UDSM*



***Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Prof. William A.L. Anangisye (wa tatu kulia) na viongozi wengine wa chuo wakimsikiliza Dkt. Mohammed Maalim (wa kwanza kushoto), Mwakilishi-Mradi wa HEET katika Taasisi ya Sayansi za Bahari (IMS) ya UDSM, iliyopo Buyu, Zanzibar wakati uongozi wa chuo ulipotembelea taasisi hiyo kuona maendeleo ya ujenzi wa majengo ya taaluma na utawala kupitia Mradi wa HEET, hivi karibuni.***

Katika hatua muhimu ya maandalizi ya hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi iliyofanyika tarehe 5 Januari 2025, Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Kapteni Hamad Bakar Hamad, alikutana na Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Prof. William Anangisye, na viongozi wengine wa chuo hicho ili kukamilisha hatua ya maandalizi ya hafla hiyo na kujadili maeneo muhimu ya ushirikiano.

Mazungumzo hayo yalifanyika katika Taasisi ya Sayansi za Baharini (IMS) iliyoko Buyu, Chukwani, Zanzibar, siku moja kabla ya hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi la jengo la shughuli za taaluma na utawala la IMS, ambayo ilihudhuriwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi.

Mkutano huu ulikuwa ni hatua muhimu katika kuimarisha mfumo wa ushirikiano kati ya Wizara na Chuo kuhusu dhamira ya pamoja ya kukuza utafiti na ushirikiano katika utafiti, ukisisitiza jukumu muhimu la UDSM katika utekelezaji wa sera za uchumi wa buluu zenye athari kwa jamii.

Kapteni Hamad Bakar Hamad alisisitiza umuhimu wa ushirikiano huu akisema, "Uchumi wa bluu ni msingi muhimu katika maendeleo endelevu ya Zanzibar. Tunathamini sana utaalamu na matokeo ya utafiti unaofanywa katika Taasisi ya Sayansi za Bahari."

Aliendelea kusisitiza akisema, "Ushirikiano huu utahakikisha kwamba sera zetu hazitategemea tu data bali pia zitazingatia mahitaji ya jamii na hatimaye kuleta athari chanya moja kwa moja katika maisha ya watu wetu."

### *Utafiti wenye Tija na wenye Kujenga Uwezo*

Prof. William Anangisye kwa upande wake alisisitiza dhamira ya UDSM katika kukuza utafiti wenye tija na wenye kujenga uwezo. Aidha, alionesha furaha yake kwa Chuo kuaminiwa na kufanya kazi kwa ushirikiano na Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi.

"Kwa pamoja, tunahakikisha kuwa matokeo ya utafiti hayaishii tu kuchapishwa katika majarida ya kitaaluma, bali yanakuwa msingi katika utungaji wa sera na ubunifu wenye manufaa kwa jamii," amesema Prof. Anangisye.

Viongozi wengine wa UDSM walioshiriki katika mkutano huo ni Prof. Bernadeta Killian, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo anayehusika na Mipango, Fedha na Utawala na Mkurugenzi wa HEET; na Prof. Saudin Mwakaje, ambaye ni Mwanasheria Mkuu wa Chuo na Katibu wa Baraza.

Prof. Killian alisisitiza wajibu wa UDSM katika kukuza rasilimaliwatu wenye ujuzi kwa ajili ya utekelezaji wa Sera ya Uchumi wa Bluu. "Dhamira yetu ni kuipatia Wizara na sekta pana ya uchumi wa buluu kwa ujumla watu wenye ujuzi na watakaofanya kazi kwa ufanisi. Ushirikiano huu ni mfano wa kuigwa wa namna ambavyo taasisi za elimu na serikali zinaweza kushirikiana ili kushughulikia changamoto zinazoweza kukwamisha maendeleo."

Miongoni mwa mambo yaliyojadiliwa ilikuwa ni namna ambavyo IMS inaweza kutoa wataalamu kwenye sekta ya uchumi wa bluu. Pande zote mbili zilikubaliana kuwa ni muhimu kipaumbele kiwekwe katika jitihada za kujenga uwezo zinazohakikisha upatikanaji wa rasilimali watu wenye ujuzi, zinazohitajika na Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi.

***Inaendelea Uk. 24***

# Rais Mwinyi Abainisha Wajibu wa IMS-UDSM katika Utekelezaji wa Sera ya Uchumi wa Bluu

*Na Jackson Isdory, HEET-UDSM*



***Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi akiwasili katika tukio la uwekaji wa jiwe la msingi la jengo la taaluma na utawala katika Taasisi ya Sayansi za Bahari (IMS) ya UDSM, Buyu, Zanzibar linalojengwa kupitia Mradi wa HEET. Rais Mwinyi ameongozana na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Prof. Adolf Mkenda na viongozi wengine. Tukio hili lilifanyika mwezi Januari, 2025.***

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, ameeleza dhamira ya Serikali yake katika utekelezaji wa Sera ya Uchumi wa Bluu kwa njia ya utafiti wa kisayansi na ubunifu.

Rais Mwinyi ameyasema hayo wakati wa hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi wa majengo mapya ya shughuli za kitaaluma na utawala katika Taasisi ya Sayansi za Bahari iliyo chini ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

"Kipaumbele cha sera yetu ni uchumi wa bluu ambao unajumuisha sekta muhimu kama vile utalii, uvuvi na kilimo cha mwani. Taasisi hii ya Sayansi za Bahari ina umuhimu wa kipekee kwani itatoa wataalamu watakaosaidia katika kuendeleza sekta hizi," alisema Rais Mwinyi.

Amesisitiza kwamba uchumi wa bluu ni msingi katika mkakati wa maendeleo wa Zanzibar, unaojumuisha utalii, uvuvi na kilimo cha mwani. Ameendelea kusisitiza kuwa utafiti wa kisayansi utakuwa nyenzo muhimu katika kuhakikisha kwamba tunakuwa na sera zinazotokana na matokeo ya utafiti kwa maendeleo endelevu.

"Tunatarajia kwamba Taasisi hii itafanya utafiti wa msingi utakaosaidia katika kuunda sera zitakazoendeleza uchumi wetu wa bluu. Lengo letu ni kuwa na sera zinazotokana na matokeo ya utafiti wa kisayansi ili kuleta maendeleo na manufaa ya muda mrefu kwa watu wetu," aliongeza Dkt. Mwinyi.

### *Shukrani kwa Serikali*

Katika hafla hiyo, Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Mhe. Dkt. Jakaya Kikwete, alitoa shukrani kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kufanikisha ujenzi wa miundombinu katika Taasisi ya Sayansi za Bahari

Majengo haya yamejengwa kwa ufadhili wa Mradi wa HEET kupitia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwa ni sehemu ya mkopo wenye masharti nafuu kutoka Benki ya Dunia.

Mafanikio haya yasingeliweza kupatikana bila uamuzi wa busara wa Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kuihusisha IMS katika Mradi wa HEET. "Uamuzi huu ulihusisha jitihada na mijadala mbalimbali lakini Mhe. Rais alinihakikishia kwamba IMS itahusishwa katika Mradi huu," ameongeza Mhe. Kikwete.

Alisisitiza kwamba kwa kawaida Benki ya Dunia kabla ya kutoa fedha za ujenzi huwa inahitaji kuwa na nyaraka halisi za umiliki wa ardhi ambapo ujenzi unafanyika. "Mheshimiwa Rais Mwinyi, tunathamini na kutambua busara zako katika kuidhinisha kutolewa kwa hati ya ardhi Buyu," amesema Mhe. Kikwete.

Mhe. Kikwete ameendelea kueleza kwamba hati ya kumiliki ardhi ni miongoni mwa nyaraka za msingi zinazopaswa kuwapo kabla ya fedha za ujenzi kuidhinishwa na Benki ya Dunia.



***Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi (katikati-waliokaa) na Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete (aliyeketi kulia kwa Rais Mwinyi) wakiwa kwenye tukio la uwekaji wa jiwe la msingi la jengo la taaluma na utawala katika Taasisi ya Sayansi za Bahari (IMS) ya UDSM, Buyu, Zanzibar linalojengwa kupitia Mradi wa HEET. Viongozi wengine ni pamoja na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Prof. Adolf Mkenda (Mb), Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Mhe. Balozi Mwanaidi Maajar, Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. William A.L. Anangisye na viongozi wengine. Tukio hili lilifanyika mwezi Januari, 2025. Picha za chini ni Bendi ya Jeshi la Polisi na kikundi kimojawapo wakitoa burudani katika tukio hilo.***

## *Upanuzi wa Elimu ya Juu*

Waziri wa Elimu, Sayansi, na Teknolojia, Mhe. Prof. Adolf Mkenda, alieleza kwamba kampasi 16 mpya za vyuo vikuu zinajengwa kote Tanzania chini ya Mradi wa HEET. Lengo ikiwa ni kufikisha elimu ya juu karibu na wananchi. Alivitaka vyuo vikuu kutoa elimu itakayolenga kuwa na wahitimu wanaoajirika na wenye ujuzi wa kukabiliana na changamoto zinazoikabili jamii hususani vijana.

Wakati huohuo Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mhe. Lela Muhamed Mussa, alieleza kwamba mitaala katika elimu ya msingi na sekondari itaboreshwa ili mbali na mambo mengine kuwe na wahitimu watakaokuwa na sifa za kujiendeleza katika mafunzo yanayohusu Sayansi ya Bahari na teknolojia ya uvuvi.

"Lengo letu ni kuhakikisha kwamba vijana wetu wanapata ujuzi wa kushiriki katika shughuli za kiuchumi zinazohusiana na bahari. Kwa mfano, watoto waliozaliwa katika maeneo kama Kojani na Tumbatu tayari wana ujuzi unaohusiana na shughuli za uvuvi; Hivyo, tunakususdia kuwapatia taaluma itakayoendana na ujuzi walionao," amesema.Mhe. Waziri.



Kwa upande wake Waziri wa Uchumi wa Bluu na Uvuvi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mhe. Shaaban Ali Othman, amesisitiza wajibu wa Chuo katika kutoa masuluhisho ya kibunifu na sera zinazotokana na matokeo ya utafiti kwa lengo la kuleta maendeleo ya Zanzibar.

"Tunahitaji sana Taasisi hii siyo tu katika upatikanaji wa rasilimaliwatu bali pia katika kuibua hoja za kitafiti na kibunifu zitakazotuwezesha kupiga hatua," amesema Mhe. Othman.

## *Kuimarisha Utafiti na Uwezo wa Taasisi*

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Prof. William A. L. Anangisye alieleza kwamba IMS imeongeza uwezo wake wa kudahili kutoka wanafunzi 140 hadi 300. Miundombinu mipya inayoongezwa itaimarisha uwezo wa taasisi katika kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu katika masuala yanayohusiana na Uchumi wa Bluu na Sayansi za Bahari.



***Inaendelea Uk. 24***

# Ujumbe wa Naibu Mratibu



## Dkt. Liberato Haule

### Naibu Mratibu wa HEET-UDSM

Kitengo cha Utekelezaji wa Mradi kinatoa shukrani za dhati kwa wadau wote wa ndani na nje ambao wamechangia katika maendeleo ya Mradi wa HEET-UDSM kama inavyoonyeshwa katika toleo hili la Jarida.

Michango ya thamani kutoka kwa wanafunzi, wafanyakazi, wakandarasi na watoa huduma imewezesha kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa mradi. Kitengo cha Utekelezaji wa Mradi kimepokea maoni kupitia njia mbalimbali, ambapo Mfumo wa Kutatua Malalamiko ndio jukwaa lililotumika zaidi.

Tunatambua jitihada za kamati za KASEMA katika kushughulikia na kutatua malalamiko, ambako ufanisi kati ya wakandarasi, wafanyakazi, watoa huduma na jamii inayozunguka umeimarishwa. Mazingira haya bora ya kazi yamekuwa chachu katika kuhakikisha kuna mafanikio katika maendeleo ya mradi.

Msaada wa vyombo vya utekelezaji na uamuzi vya UDSM, ikiwamo Kamati ya Usimamizi wa Mradi, Bodi ya Zabuni ya UDSM, Kamati za Usimamizi, Seneti na Kamati za Baraza, umekuwa na umuhimu mkubwa. Mapendekezo na miongozo yao vimechangia kwa kiasi kikubwa katika utekelezaji wa mafanikio ya mradi huu.

Kitengo cha Utekelezaji wa Mradi pia kinazishukuru Benki ya Dunia na Serikali ya Tanzania kwa msaada mkubwa. Benki ya Dunia imetoa miongozo, idhini na msaada wa kiufundi wakati wote wa utekelezaji wa mradi, huku Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Wizara ya Fedha zikiwezesha michakato muhimu, ikiwamo kutoa kipaumbele katika madai ya kifedha yanayohusiana na mradi huu.

Tunapenda kutoa pongezi maalumu kwa Ofisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na Mkaguzi Mkuu wa Ndani kwa ziara zao za ushauri ambazo zimeimarisha usimamizi na ufuatiliaji katika utekelezaji wa mradi. Pia, tunathamini ziara za kubadilishana maarifa kutoka kwa taasisi zingine zinazotekeleza miradi ya HEET, kwa kuwa kupitia ziara hizo, tunajifunza mengi ambayo mbali na mambo mengine yanachochea katika uboreshaji wa utekelezaji wa shughuli za Mradi.

Tunatarajia kuhusisha taasisi nyingi zaidi na kuendeleza ushirikiano kadiri tunavyoendelea na Mradi wa HEET UDSM. Ninawatakia usomaji mwema!

# Tahariri

## UDSM kuwa Kinara wa Mageuzi katika Uchumi wa Bluu na Teknolojia Maizi

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kimeendelea kuthibitisha nafasi yake kama kinara katika masuala ya elimu ya juu, utafiti na ubunifu kupitia uwekezaji wa mkakati katika maeneo muhimu yanayoendana na ajenda za maendeleo za kitaifa na kimataifa. Toleo hili la Jarida la HEET mbali na mambo mengine linajivunia kubainisha hatua muhimu zinazochukuliwa na Chuo Kikuu katika kuunga mkono mkakati wa uwekezaji katika uchumi wa bluu, kukuza teknolojia maizi na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kutumia teknolojia ya kidijiti.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, hivi karibuni alibainisha wajibu wa UDSM katika mchakato wa uundaji wa Sera ya Uchumi wa Bluu. Aidha, alisisitiza kuhusu mchango wa UDSM katika sekta hii muhimu. Kupitia Taasisi ya Sayansi za Bahari (IMS), UDSM iko mstari wa mbele katika utafiti na jitihada za kujenga uwezo ambazo zitachangia katika matumizi endelevu ya rasilimali za bahari.

Mpango wa UDSM katika kushirikiana na Wizara ya Uchumi wa Bluu, Zanzibar, unasisitiza zaidi juu ya umuhimu wa jitihada hizi. Haya yamedhihirika wakati wa hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi katika ujenzi wa jengo la utawala na masuala ya taaluma katika Taasisi ya Sayansi za Bahari. Ujenzi huu unaofadhiliwa na Benki ya Dunia kupitia Mradi wa HEET unadhihirisha dhamira ya dhati ya serikali katika kukuza sekta ya bahari inayokua kwa kasi hapa nchini.

Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne, Mhe. Jakaya Kikwete, alibainisha mwelekeo wa UDSM kuelekea kuwa Kituo Mahiri katika masuala ya Utafiti wa Sayansi za Bahari barani Afrika. Kwa kuzingatia uwekezaji katika masuala ya utafiti na uendeshaji wa programu mbalimbali za kitaaluma, UDSM imedhamiria kuwekeza katika kukuza maarifa na ubunifu ambao utakuwa na manufaa kwa jamii ndani na nje ya Tanzania pamoja na kutoa maarifa na ubunifu ambao utainufaisha Tanzania na bara zima la Afrika. Uunganishaji wa jitihada hizi na sera za kitaifa unahakikisha kwamba utafiti unaofanywa UDSM utachangia moja kwa moja katika mageuzi ya kiuchumi.

Mbali na uwekezaji katika masuala yanayohusiana na sayansi za bahari, UDSM imepiga hatua kubwa katika mageuzi ya kidijiti. Uwekaji wa miundombinu ya msingi ya mtandao, ikiwa ni pamoja na mtandao wa faiba na kuweka swichi chini ya Mradi wa HEET UDSM, unaleta mapinduzi katika uunganishaji wa mtandao katika Kampasi za UDSM. Maendeleo haya yanaweka msingi wa upatikanaji wa intaneti yenye kasi kubwa, kuimarisha ushirikiano na shughuli za utafiti na ujifunzaji.

Jambo la msingi la kuzingatia katika mapinduzi haya ya kiteknolojia ni juhudi za Chuo katika kujenga mazingira ya kuwa na kampasi maizi ya kufundishia na kujifunzia. Uwekezaji katika teknolojia za madarasa maizi, mfumo wa pamoja wa mtandao pamoja na mfumo wa baruapepe ili kuimarisha ushirikiano, pamoja na uandaaji wa sera ya elimu mtandao ni hatua muhimu ya kutoa elimu kwa mifumo ya kisasa. Jitihada hizi zinahakikisha kwamba wanafunzi na wahadhiri wanapata fursa ya kujenga uzoefu wa kitaaluma katika mfumo jumuishi na wenye ufanisi.

Mabadiliko haya yanajumuisha Mifumo ya Taarifa za Kijiografia (GIS) na teknolojia maizi, ambapo UDSM inasimamia ubunifu katika usimamizi wa data na uchambuzi wa kijiografia. Aidha, kukamilika kwa uwezo mkubwa wa maltimedia katika kampasi zote kunadhihirisha dhamira ya Chuo katika kutumia zana za kidijiti kwa ajili ya utafiti na usambazaji wa maarifa.

Kwa maendeleo haya ya kipekee, UDSM inatekeleza dhamira yake ya kuwa kitovu katika utoaji wa elimu, utafiti, na ubunifu ndani na nje ya Tanzania. Maeneo muhimu yanayoangaziwa ambayo ni pamoja na utafiti katika masuala yanayohusiana na sayansi za bahari, uunganishaji wa mifumo ya dijitali na teknolojia maizi yanaifanya UDSM kuwa kituo mahiri katika mabadiliko ya kiuchumi.

Maendeleo haya makubwa yanayofanywa na UDSM yanadhihirisha mchango wa taasisi za elimu ya juu katika kuboresha mustakabali wa kitaifa na kimataifa.

HEKIMA NI UHURU

HEET
HIGHER EDUCATION FOR ECONOMIC TRANSFORMATION


### Uratibu wa Mradi wa HEET-UDSM

**Mratibu wa Mradi**
Prof. Bernadeta Killian

**Naibu Mratibu wa Mradi**
Dkt. Liberato V. Haule

### Timu ya Uhariri

**Mhariri Mkuu &**
**Mtaalamu wa Uhusiano kwa Umma na Mawasiliano HEET-UDSM**
Dkt. Dotto Paul Kuhenga

**Waharir**i
Dkt. Lupa Ramadhani (Kiingereza)
Dkt. Mussa Hans (Kiswahili)

**Waandishi:**
Jackson Isdory
Zamda George
Ally Mambele
Mercy Machange
Remmy Wilson

**Mpiga Picha:**
Tumaini Kibangala

**Msanifu**
Michael Mwakatobe




# Matukio katika Picha

***Matukio mbalimbali wakati wa kuwekwa kwa jiwe la msingi la jengo la taaluma na utawala katika Taasisi ya Sayansi za Bahari (IMS), ya UDSM, Buyu, Zanzibar linalojengwa kupitia Mradi wa HEET Januari, 2025.***





*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi*



*Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete*




*Mhe. Prof. Adolf Mkenda (Mb), Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia*





*Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Prof. William A. L. Anangisye*




Zanzibar
Pingwe
Paje
Kizimkazi
Mkunguni
Kisiwa





# Sera ya Ujifunzaji Mtandaoni UDSM Yazinduliwa

*Na Ally Mambele, HEET-UDSM*

Katika jitihada zake za kuwa kinara wa mageuzi makubwa katika elimu ya juu nchini Tanzania, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kinaandaa sera ya maendeleo ya ujifunzaji mtandaoni ili kuendeleza elimu kidijiti, iliripotiwa.

Jitihada hizi zinazofadhiliwa na Mradi wa HEET, zinatarajiwa kuleta mapinduzi katika ufundishaji, ujifunzaji, na utafiti kwa kuboresha usambazaji wa maudhui ya kidijiti, kupanua wigo wa upatikanaji wa elimu ya ubora, na kujumuisha mbinu za ufundishaji zinazoongozwa teknolojia.

Kwa mujibu wa Mtaalamu wa Elimu na Teknolojia ya Kidijiti wa Mradi wa HEET-UDSM, Dkt. Kwame Ibwe, sera hii imeandaliwa kwa kufanya uchambuzi mpana wa mbinu bora tulizojifunza kutoka vyuo vikuu 15 vinavyoongoza duniani.

"Mbinu bora katika muktadha huu zilihusisha ziara ya ulingalishi viwango kutoka vyuo na taasisi zilizopo Marekani, India, Afrika Kusini, Kenya, na Naijeria. Utafiti huu ulilenga kuchunguza upatikanaji wa miundombinu ya kidijiti, ubora wa maudhui, mifumo ya udhibiti na uendelevu ili kuhakikisha kuwa mifumo ya UDSM licha ya kuzingatia mfumo wa elimu nchini Tanzania, inaendana na viwango vya kimataifa," alisema Dkt. Ibwe.

Maeneo Makuu ya Sera ya Ujifunzaji Mtandaoni

Aidha, alibainisha kuwa maeneo muhimu ya Sera ya Ujifunzaji Mtandaoni yalijumuisha kuboresha upatikanaji na ujumuishi, ambapo sera hii itahakikisha rasilimali za ujifunzaji mtandaoni zinapatikana kwa wanafunzi wote, ikiwa ni pamoja na wenye ulemavu na walio katika maeneo ya vijijini, kupitia teknolojia saidizi na vituo vya kikanda vya kujifunzia.

Dkt. Ibwe alieleza pia kuhusu uwekezaji katika miundombinu na teknolojia kama eneo lingine muhimu la sera hii, ambapo UDSM imepanga kuboresha Mfumo wa Usimamizi wa Ujifunzaji (LMS), kupanua wigo wa upatikanaji wa intaneti katika kampasi zote, na kuanzisha maktaba za kidijiti ili kusaidia ujifunzaji mtandaoni.

"Vilevile, maudhui ya sera hii yanajumuisha kujengea uwezo wa wanataaluma na wafanyakazi ambapo wanataaluma watapatiwa mafunzo maalumu ya uandaaji wa maudhui ya kidijiti, ufundishaji mtandaoni na matumizi ya teknolojia zinazoibuka ili kuboresha ufanisi katika ufundishaji," alisema.

Aliongeza akisema, "Sera hii pia inajumuisha ufadhili na ushirikiano endelevu, ikizingatiwa kwamba Chuo kinakusudia kukuza ushirikiano na sekta binafsi, kunufaika na ufadhili wa serikali na mapato yanayotokana na mafunzo ya kozi fupi za mtandaoni ili kusaidia katika ukuaji endelevu wa ujifunzaji mtandaoni."

"Sera hii pia inajumuisha udhibiti wa ubora na uandaaji wa maudhui, ujumuishaji wa mifumo madhubuti ya ufuatiliaji wa ubora ili kuhakikisha kwamba maudhui ya ujifunzaji mtandaoni yanakidhi viwango vya kitaaluma, yanakuwa shirikishi, na yanayoimarisha matokeo ya ujifunzaji," alisisitiza.



***Mfumo Madhubuti wa Ujifunzaji Mtandaoni***

Kiongozi wa timu ya uandaaji sera, Prof. Abdi T. Abdallah wa Ndaki ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano UDSM, alisisitiza umuhimu wa mfumo madhubuti wa ujifunzaji mtandaoni, unaoongozwa na utafiti na unaoweza kuendana na mabadiliko.

"Ufanisi wa sera hii unategemea uwezo wake wa kuwezesha ujifunzaji wa kiwango cha juu, huku ukiendelea kuwa endelevu. Ni lazima tuhakikishe kuwa majukwaa yetu ya ujifunzaji kidijiti si tu yanapatikana, bali pia yana ufanisi katika kutoa elimu yenye athari chanya," alisema Prof. Abdallah.

Prof. Abdallah pia alisisitiza umuhimu wa kuhakikisha kuwa wanataaluma wanakuwa na ujuzi wa kutosha wa kufundisha mtandaoni, akibainisha, "Mafunzo na ujengeaji uwezo unapaswa kuwa endelevu, na motisha inapaswa kutolewa ili kuhamasisha ubunifu katika kuandaa maudhui ya kujifunza kidijiti."


Hatua hii ni sehemu ya Dira ya UDSM ya 2061, inayolenga kukifanya Chuo kuwa kinara wa elimu kidijiti katika kanda. Kwa kutumia mikakati ya hali ya juu ya ujifunzaji kidijiti, UDSM siyo tu inaimarisha uwezo wake wa kufundisha na utafiti, bali pia inakuza ushirikiano wa kimataifa ambao utaimarisha athari zake kitaaluma.

Mara baada ya sera hii kutekelezwa kikamilifu, inatarajiwa kuongeza usajili wa wanafunzi katika programu za mtandaoni, kuongeza fursa za kujifunza na kuunda mfumo wa elimu unaoendana na mabadiliko, maendeleo ya kiteknolojia, na mahitaji ya elimu yanayoibuka kila uchao.

Sera hii imelenga kuboresha matokeo ya ujifunzaji na kupanua wigo wa upatikanaji wa elimu ya juu. Kupitia Mradi wa HEET, mfumo imara wa kujifunza kidijiti unatekelezwa ili kuhakikisha uendelevu wa muda mrefu wa jitihada za ujifunzaji mtandaoni.

# Kampasi Maizi yaanza UDSM kwa Uunganishaji na Usambazaji wa Mkongo wa Mtandao

*Na Mercy Machange, HEET-UDSM*



***Ufungaji wa nyaya za mawasiliano katika mtandao mkuu ukiweka msingi wa miundombinu ya kampasi mahiri yenye kasi na uimara wa mawasiliano katika UDSM***

Katika jitihada za kuimarisha uunganishaji wa kidijiti na kuboresha mifumo ya ufundishaji na ujifunzaji, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa sasa kinaunganisha mkongo wa mawasiliano katika kampasi zake ili kuimarisha usambazaji na upatikanaji wa mtandao kupitia Mradi wa HEET.

Jitihada hizo kupitia mradi huu unaofadhiliwa na Benki ya Dunia ni sehemu ya mpango wa kuwa na kampasi maizi ya UDSM, unaolenga kuboresha miundombinu ya TEHAMA ili kuimarisha uunganishaji wa mtandao na kuboresha mifumo ya ufundishaji na ujifunzaji.

"Jitihada hizi pia zinalenga kuimarisha miundombinu na huduma za kidijiti pamoja na kuanzisha mfumo wa usimamizi wa rasilimali za taasisi (ERMS)," anaeleza Dkt. Kwame Ibwe, Mtaalamu wa Elimu na Teknolojia ya dijitali wa Mradi wa HEET- UDSM.

Dkt. Ibwe alisema kuwa mchakato wa uunganishaji unaendelea kama ilivyopangwa na unatarajiwa kukamilika ifikapo Desemba, 2025.

"Baada ya kukamilika, miundombinu iliyoboreshwa itaimarisha kwa kiasi kikubwa muunganiko wa maeneo muhimu ya Chuo, zikiwamo kumbi za mihadhara, maktaba, majengo ya utawala na hosteli za wanafunzi," alisema Dkt. Ibwe.

Aliongeza kuwa usambazaji na upatikanaji wa mitandao ni vipengele muhimu vya TEHAMA ambavyo timu ya wataalamu dijitali inavishughulikia kwa sasa. "Kwa sasa, michakato yote inaendelea vizuri, vipimo vya kiufundi na makadirio ya gharama vimekamilika na hatua inayofuata ni kuwaalika wazabuni kupitia mchakato wa zabuni ya wazi. Tunatarajia kuwa ifikapo Desemba, 2025, uunganishaji utakuwa umekamilika na kuanza kutumika," aliongezea Dkt. Ibwe.

### *Kuimarisha Mchakato wa Ujifunzaji na Utafiti*

Katika kuunga mkono ujifunzaji wa kidijitali, kupitia jitihada hizi, UDSM inaimarisha majukwaa yake ya mtandaoni, yakiwamo LMS Moodle na MOOC, ambayo yatamrahisishia mwanafunzi kutumia rasilimali za kielimu.

Dkt. Ibwe alibainisha kuwa studio za maltimedia zimeanzishwa katika Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia (CoET) na Ndaki ya Teknolojia za Habari na Mawasiliano (CoICT) ili kuwezesha uandaaji na usambazaji wa maudhui ya kidijiti. Mtandao mpya wa data za TEHAMA utaimarisha shughuli za kitaaluma na kiutawala chuoni.

"Kwa mtandao ulioboreshwa, wanafunzi, wafanyakazi na watafiti watapata intaneti ya kuaminika kwa ajili ya shughuli za ujifunzaji, utafiti, na ushauri," alieleza Dkt. Ibwe.

### *Miundombinu ya Didijitali Inayoendana na Mabadiliko Kusaidia zaidi ya Watumiaji 50,000*

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kinaboresha miundombinu yake ya kidijiti ili kuwasaidia zaidi ya watumiaji 50,000 na kuhakikisha uzoefu wa hali ya juu wa kidijiti katika kampasi za UDSM unafikiwa kwa ufanisi. Mbali na elimu, mtandao huu ulioboreshwa utawezesha teknolojia zinazoibuka kama vile uunganishaji wa akiliunde, mifumo ya taarifa za kijiografia na mifumo ya kuhifadhi data mtandaoni.

Dkt. Ibwe alisisitiza umuhimu wa kuboresha mtandao, akisema, "Tunatarajia kupokea ongezeko kubwa la mtandao kutoka SEACOM na TERNET. Zaidi ya 80% ya mtandao utatolewa kwa vitengo mbalimbali vya chuo ili kuboresha muunganisho na huduma za kidijiti."

Uunganishaji wa mkongo ulioboreshwa kutoka kwenye mtandao mkuu hadi vitengo hivi utafanya kazi kwa kasi ya Gbps 40 ili kuhakikisha upatikanaji wa haraka na wa kuaminika kadiri idadi ya watu wa chuo inavyoongezeka. "Uboreshaji huu unatarajiwa kutoa uzoefu bora wa mtumiaji, ukiwezesha upatikanaji usio na vikwazo wa rasilimali za dijitali katika kampasi yote," alisisitiza Dkt. Ibwe.

Kupitia jitihada hizi, UDSM inaimarisha mpango wake wa kuwa na kampasi maizi, ikikuza ubunifu, ufanisi na mazingira bora ya ujifunzaji wa kidijiti kwa ustawi wa wanafunzi na wafanyakazi.

# Teknolojia ya Kisasa Kuifanya UDSM Kinara katika Mabadiliko ya Dijitali ya Elimu ya Juu

*Na Zamda George, HEET-UDSM*




Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kipo katika hatua kubwa za maendeleo ya teknolojia kwa kuunganisha Mifumo ya Taarifa za Kijiografia (GIS) na teknolojia maizi ili kukuza utafiti, ujifunzaji na usimamizi wa mazingira. Mradi wa HEET unaochochea mabadiliko haya, unatarajiwa kuleta maendeleo makubwa katika mpango wa Chuo Kikuu cha Kampasi Maizi.

Dkt. Kwame Ibwe, Mtaalamu wa Elimu na Teknolojia ya Dijitali wa Mradi wa HEET -UDSM, alisisitiza umuhimu wa maendeleo haya. "Tunaingia katika enzi ambapo Mifumo ya Taarifa za Kijiografia na ujifunzaji kwa njia ya mtandao siyo tu vitaboresha utafiti wa kitaaluma, bali pia vitatoa suluhisho halisi katika maeneo mbalimbali kama mipango miji, uhifadhi wa mazingira na kujiandaa kukabiliana na majanga."

Dkt. Ibwe alisema, "Mojawapo ya maendeleo yanayosubiriwa ni uunganishaji wa Mifumo ya Taarifa za Kijiografia kwa njia ya mtandao kwa lengo la kuimarisha uainishaji wa matumizi na tabaka ardhi."

"Maendeleo haya yatawawezesha watafiti na wanafunzi kuchambua kiasi kikubwa cha data za kijiografia kwa usahihi wa hali ya juu. Maendeleo yatabadilisha kabisa namna tunavyoeleza mabadiliko ya mazingira na kujiandaa kwa changamoto za siku zijazo," alibainisha Dkt. Ibwe.

Aliongeza kuwa, mbali na uchoraji ramani na uainishaji maeneo, UDSM pia inajikita katika uchanganuzi wa utabiri kwa kutumia akiliunde. Kwa kuchambua data za kihistoria na za muda halisi, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinalenga kuunda modeli za utabiri wa mwenendo wa mazingira.

"Lengo letu ni kuunda zana za utabiri zitakazowasaidia wahandisi kusanifu miundombinu himilivu zaidi, kuboresha matumizi ya ardhi na kuimarisha mifumo ya kukabiliana na majanga," alieleza Dkt. Ibwe.

### *Kuimarisha Utafiti na Ujifunzaji kupitia Teknolojia Maizi*

Mkurugenzi wa Kurugenzi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano UDSM, Dkt. Salome Maro, aliongeza kuwa uanzishwaji wa teknolojia hizi unatarajiwa kubadili kabisa uzoefu wa utafiti na ujifunzaji katika UDSM.

"Vifaa maizi vitapatikana kwa wanafunzi na wafanyakazi wa chuo hivi karibuni, ambapo vitatoa fursa ya uchangamani katika masomo yanayoongozwa na data. Maendeleo haya siyo tu kwamba yataboresha uwezo wa utafiti, bali pia yatakifanya UDSM kuwa kinara katika ubunifu wa kidijitali barani Afrika," alisema Dkt. Maro.

Kwa maendeleo haya, UDSM inajizatiti kuimarisha ubora wa kitaaluma na hatimaye kuwa na athari kwa jamii. Mageuzi katika Mifumo ya Taarifa za Kijiografia na teknolojia maizi yanatarajiwa kusaidia jitihada za kitaifa na kimataifa katika uhifadhi wa mazingira, maendeleo endelevu na mipango miji.

"Tunapojiandaa kutekeleza ubunifu huu, mustakabali wetu unaonekana kuwa na matumaini makubwa kwa wanafunzi, watafiti na wataalamu wetu ambao watatumia Mifumo ya Taarifa za Kijiografia na teknolojia maizi kutatua changamoto halisi za dunia," alisisitiza Dkt. Maro.

Mradi wa HEET umejikita katika kukuza mfumo wa ikolojia unaoongozwa na teknolojia unaohakikisha UDSM inabaki kuwa kinara katika mabadiliko ya dijitali katika elimu ya juu.

# Waziri Jafo asisitiza ubiasharishaji wa matokeo ya utafiti na kuzingatia ustawi wa jamii

*Na Jackson Isdory, HEET-UDSM*




***Dkt. Selemani Said Jafo, Waziri wa Viwanda na Biashara akiongea wakati wa kufunga warsha ya ubiasharishaji wa utafiti iliyofanyika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hivi karibuni***

Katika wito unaopaswa kupewa kipaumbele, Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Dkt. Selemani Saidi Jafo (Mb), amekitaka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kuongeza jitihada katika utafiti na ubunifu kwa kuzingatia ustawi wa jamii pamoja na kubiasharisha matokeo ya kazi zinazotokana na utafiti.

Akizungumza katika hitimisho la warsha ya kimkakati ya siku nne kuhusu ubiasharishaji wa utafiti iliyofanyika kuanzia tarehe 25 hadi 28 Machi 2025, Dkt. Jafo alisisitiza umuhimu wa kutumia matokeo ya tafiti za kitaaluma ili kupata masuluhisho endelevu na yenye tija yatakayowanufaisha wananchi moja kwa moja.

"Utafiti na ubunifu ni nyenzo muhimu kwa mabadiliko ya kijamii. UDSM inapaswa kuwa kinara katika kubadilisha maarifa kuwa matokeo halisi yenye kugusa maisha ya jamii," alisema Dkt. Jafo, akiwahimiza wasomi kujikita katika matokeo yanayoshughulikia mahitaji halisi ya jamii.

Alimpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa uongozi wake wa kuona mbali katika kuunga mkono elimu ya juu na utafiti, hususan kupitia Mradi wa HEET. "Jitihada zake zimeifungulia nchi yetu fursa za uwekezaji, diplomasia, na maendeleo ya kisayansi," aliongeza.

Waziri Jafo alisisitiza umuhimu wa kulinda milikidhihini na kuwasihi wabunifu kusajili kazi zao kupitia BRELA ili kulinda umiliki na kuongeza tija ya kiuchumi. Pia, alizihimiza sekta za viwanda kushirikiana na wabunifu hususani vijana kupitia progaramu za mafunzo kazini na kushirikiana katika kutengeneza vielelezo muafaka, kuandaa wahitimu wenye ujuzi wa kazi na kuendeleza utafiti wa kivitendo.

Mhe. Balozi Mwanaidi Maajar, Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, akiunga mkono hoja ya Mhe. Waziri alisema: "Utafiti usio na matokeo ni fursa iliyopotea. Tumejizatiti kuimarisha mifumo ya taasisi inayounga mkono ubunifu wenye tija".

*Inaendelea Uk. 25*



***Mhe. Dkt. Selemani Said Jafo (Mb), Waziri wa Viwanda na Biashara (wa pili kushoto) akisikiliza maelezo kutoka kwa mmoja wa watafiti wakati wa warsha ya ubiasharishaji wa utafiti iliyofanyika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hivi karibuni. Wengine kwenye picha, kushoto kwa Waziri ni Mwenyekiti wa Baraza la Chuo, Mhe. Balozi Mwanaidi Maajar, Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. William A.L. Anangisye na Naibu Makamu Mkuu wa Chuo-Taaluma, Prof. Bonaventure Rutinwa.***

# Benki ya Dunia yatoa wito wa kuharakisha utekelezaji wa shughuli za Mradi wa HEET huku UDSM ikionyesha maendeleo ya kupigiwa mfano

*Na Tumaini Kibangala, HEET-UDSM*



*Kiongozi Mkuu wa Kimataifa wa Elimu ya Juu katika Benki ya Dunia ambaye pia ni Kiongozi wa Timu ya Utekelezaji Bi. Roberta Malee Bassett (katikati) akiongea na baadhi ya viongozi kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na wawakilishi wa taasiai mbalimbali za elimu ya juu (tazama picha ya chini) zinazotekeleza Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Uchumi (HEET), hivi karibuni, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kushoto kwake ni Mkurugenzi wa Elimu ya Juu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Peter Msofe, na kulia kwake ni Mtaalamu wa Elimu Mwandamizi na Kiongozi Mwenza wa Timu ya Utekelezaji katikaBenki ya Dunia Bw. Kaboko Nkahiga.*

Kadri Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinavyoshuhudia maendeleo ya kupigiwa mfano katika utekelezaji wa Mradi wa HEET, Benki ya Dunia imetoa wito kwa taasisi za elimu ya juu zinazotekeleza mpango huu kuharakisha maendeleo ya miundombinu na kuboresha usimamizi wa miradi.

Wito huu, ulitolewa kutokana na kasi ndogo ya maendeleo ya ujenzi katika baadhi ya taasisi, katika mkutano uliofanyika hivi karibuni katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), ukiwakutanisha kwa pamoja maofisa kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, wawakilishi wa Benki ya Dunia, na viongozi kutoka taasisi za elimu ya juu zinazotekeleza Mradi wa HEET nchini Tanzania.

Mkutano ulianza na kikao kilichoongozwa na Prof. Carolyne Nombo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, akipokea ripoti ya taifa kuhusu maendeleo ya utekelezaji katika maeneo mbalimbali ya Mradi wa HEET.

Akizungumza katika kikao hicho, Bwana Nkahiga Kaboko, mwakilishi wa Benki ya Dunia, alisisitiza umuhimu wa taasisi za elimu ya juu kusimamia kwa karibu wakandarasi ili kuhakikisha shughuli za ujenzi zinakamilika kwa wakati, badala ya kusubiri nyongeza za muda wa Mradi.

"Ni muhimu taasisi ziimarishe usimamizi wa wakandarasi ili shughuli za ujenzi zikamilike kwa wakati, kulingana na malengo ya Mradi," alisisitiza Bwana Kaboko.

Akisisitizia suala hilo, Dkt. Peter Msofe, Mkurugenzi wa Elimu ya Juu katika Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, alithibitisha dhamira ya serikali ya kusimamia kwa karibu utekelezaji wa mradi wa HEET. Aliwataka wadau wote wanaohusika kusimamia mradi kikamilifu ili kuhakikisha kwamba wakandarasi wanatekeleza majukumu yao kama ilivyoainishwa kwenye mikataba yao.


"Fanyeni kila linalowezekana kuboresha usimamizi na ufuatiliaji wa wakandarasi ili kuhakikisha kwamba wanakamilisha kazi ndani ya muda uliopangwa. Kasi ya ujenzi katika taasisi nyingi bado hairidhishi, na muda unayoyoyoma ikizingatiwa kuwa muda wa ukomo wa mradi ni Juni 2026," alisisitiza Dkt. Msofe.

***Inaendelea Uk. 25***



# Mabadiliko makubwa katika Miundombinu ya TEHAMA na Teknolojia Maizi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM)

*Na Ally Mambele, HEET-UDSM*




*Ufungaji wa mifumo ya udhibiti wa kuingia kwa njia ya kisasa katika mtandao mkuu—kuboresha usalama na udhibiti wa upatikanaji ndani ya miundombinu ya kampasi mahiri*

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kinapiga hatua kubwa katika mageuzi ya kidijitali kwa kuboresha miundombinu yake ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ili kuimarisha uwezo wa elimu ya dijitali na kukuza mazingira maizi ya ujifunzaji kupitia Mradi wa HEET.

Wakati wa wasilisho la hivi karibuni kuhusu maendeleo ya mpango wa dijitali wa UDSM, Mtaalamu wa Elimu na Masuala ya ijit wa HEET- UDSM, Dkt. Kwame Ibwe, alieleza kwa kina kuhusu mpango huu unaoendelea na kusisitiza jukumu muhimu la teknolojia katika kuhakikisha uendelevu wa ujifunzaji na uhimilivu wa taasisi.

“Ufanisi wa vyuo vikuu vya kisasa unategemea uwezo wa kutumia teknolojia maizi katika ufundishaji, utafiti na utawala. Uwekezaji wa UDSM katika miundombinu ya kidijiti si maboresho tu, bali ni mageuzi ya kuelekea kuwa kampasi maizi ya dijitali, inayoendana na mabadiliko,” alisema Dkt. Ibwe.

Alifafanua zaidi kuwa kiini cha mageuzi haya ni Kampasi Maizi ya UDSM, wazo la kuwa na miundombinu ya mtandao wa kisasa na vifaa vinavyounganishwa na intaneti ili kuboresha utawala, ufundishaji, utafiti na ushirikishwaji wa wanafunzi.

“Kampasi maizi inaunganisha watu, vifaa na programu, ikiruhusu ufanyaji uamuzi unaotokana na takwimu kwa ajili ya kuboresha ufanisi, usalama na matumizi sahihi ya rasilimali,” alisema Dkt. Ibwe.

Dkt. Ibwe alisema kuwa miongoni mwa maeneo muhimu ya uwekezaji wa kidijitali kwa UDSM ni uboreshaji wa miundombinu ya TEHAMA, ambapo Chuo kimeanza maboresho makubwa ya mifumo yake mikuu, usambazaji na upatikanaji wa mtandao. “Hii inajumuisha uunganishaji wa mifumo yenye kasi ya kiwango cha juu, mifumo mipya ya usalama na uboreshaji wa muunganiko katika kampasi zote,” alisema.

Eneo lingine ambalo UDSM inawekeza ni katika kuboresha mifumo ya ujifunzaji wa kidijitali, ambapo Chuo kinaimarisha Mfumo wa Usimamizi wa Ujifunzaji (LMS), Moodle, pamoja na jukwaa la Mafunzo Huria Mtandaoni kwa Wengi (MOOC) ili kuunga mkono ujifunzaji unaoendana na mabadiliko.

“Pia, Chuo kinawekeza katika studio za maltimedia kwa ajili ya uandaaji wa maudhui ya dijitali, ambapo studio za kisasa katika Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia (CoET) na Ndaki ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (CoICT) zitasaidia katika uzalishaji wa nyaraka za elimu za ubora wa juu kwa kozi za mtandaoni na mseto,” alisema.



Ameongeza, “Tunalenga pia kuwekeza katika teknolojia za kisasa kama akiliunde na Mifumo ya Taarifa za Kijiografia (GIS), ambazo zinaunganishwa kwenye ujifunzaji wa kidijitali ili kuimarisha utafiti na uchanganuzi wa data. Tunaanzisha Kadi Maizi za Utambulisho *(Smart ID Cards)* na kuziunganisha na huduma za dijitali ili kuboresha udhibiti wa upatikanaji, usimamizi wa maktaba na huduma kwa wanafunzi.”

Dkt. Ibwe alisema kuwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pia kinawekeza katika miundombinu ya kompyuta na ya hifadhi, ikiwa ni pamoja na ununuzi wa seva za kisasa za baruapepe na suluhisho la mifumo ya kuhifadhi data mtandaoni (cloud) ili kuhakikisha usalama wa data na kurahisha mawasiliano pamoja na kuwa na chumba cha mitihani mtandaoni ambacho kinajumuisha mfumo wa usimamizi wa mitihani ulio salama na unaotumia teknolojia ili kuwezesha upimaji wa kimasafa.

“Kwa muktadha huu, kwa ujumla, Mradi wa HEET UDSM siyo tu kwamba unalenga kufanya upanuzi wa kidijitali, bali pia unakusudia kujizatiti kwa mustakabali wa UDSM dhidi ya changamoto zinazoweza kujitokeza kama ilivyotokea wakati wa ugonjwa wa UVIKO-19,” alisisitiza.

Alisema kwamba ahadi ya Chuo katika kutumia mbinu bunifu za ufundishaji, kuimarisha utafiti wa vitendo (tumizi) na kutengeneza mazingira ambapo wanafunzi na wahadhiri wanaweza kustawi katika dunia inayotumia teknolojia, inatimia.

Kupitia uwekezaji huu wa kimkakati wa kidijitali, UDSM inajiweka katika nafasi ya kuwa kinara katika mabadiliko ya elimu ya juu ikitengeneza fursa ya uzoefu wa mustakabali wa utayari wa kujifunza unaotumia teknolojia.





*Kituo kipya cha mtandao mkuu chenye vifaa vya mtandao vilivyowekwa katika makabati maalum kikiwa na miundombinu imara ya umeme ikijumuisha UPS na jenereta ya dharura kwa kuhakikisha uendeshaji usiokatizwa*







## Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi, UDSM Wakutana katika Maandalizi ya Hafla ya Kihistoria ya Uwekaji wa Jiwe la Msingi IMS



*Inatoka Uk. 10*

Prof. Saudin Mwakaje aliishukuru Wizara kwa msaada na dhamira yake katika jitihada za kuimarisha ushirikiano. "IMS inaendelea kuwa kinara katika kufanya utafiti katika kanda hii. Msaada unaoendelea kutolewa kutoka katika Wizara na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ujumla ni hatua muhimu katika kudumisha ubora huu na kukuza ushirikiano kwa pande zote unaonufaisha wadau wote," alisisitiza Prof. Mwakaje.

### *Matokeo ya Jitihada za Ushirikiano*

Viongozi wa UDSM waliishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi kwa msaada thabiti na uongozi wa madhubuti wenye maono, ambao ni muhimu katika kuimarisha ushirikiano huu ambao umekuwa mfano wa ushirikiano kati ya serikali na taasisi za elimu katika kanda hii.

Kuhusu hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi iliyofanyika tarehe 5 Januari 2025, walieleza kwamba itakuwa ni ushahidi wa juhudi hizi za ushirikiano na maono yao ya pamoja ya uchumi wa bluu endelevu na wenye mafanikio. Hatua hii ya kihistoria itazidi kuimarisha uhusiano kati ya Wizara na Chuo, huku ikifungua ukurasa wa mafanikio makubwa zaidi kwa baadaye.

## Rais Mwinyi Abainisha Wajibu wa IMS-UDSM katika Utekelezaji wa Sera ya Uchumi wa Bluu

*Inatoka Uk. 12*

"Tuko katika hatua nzuri ya kukamilisha Mradi kwa wakati ikizingatiwa kwamba ujenzi umekamilika kwa 50% na kwamba ShT. bilioni 4.2 zimekwishatolewa kwa mkandarasi. Tunatarajia kukamilisha Mradi kwa wakati, hivyo, manufaa yake yataanza kuonekana hivi punde," amesema Prof. Anangisye.

Mwakilishi mkazi wa Benki ya Dunia, Bw. Martin Kachingwe, ameipongeza Serikali kwa jitihada zake katika elimu na maendeleo na kusisitiza umuhimu wa ushirikiano baina ya serikali, vyuo na wadau.

"Mradi wa HEET unalenga kutoa fursa ya elimu kwa wote hususani kwa jamii za pembezoni. Mradi huu unaviwezesha vyuo vikuu kama UDSM kujiimarisha katika elimu, utafiti na ubunifu utakaosaidia katika kuinua uchumi wa taifa. Tunaamini kwamba uwekezaji huu utawanufaisha wanafunzi katika mustakabali wa maisha yao," amesema Bw. Kachingwe.

Kupitia utafiti, ukuzaji wa uwezo na ushirikiano, UDSM imetoa mchango mkubwa katika kukabiliana na changamoto na utafutaji wa fursa katika sekta ya uvuvi na ufugaji wa samaki nchini Tanzania. Mpango huu unasisitiza dhamira ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla katika kutumia rasilimali za bahari kwa njia endelevu kwa lengo la kuhamasisha kwamba maendeleo ya kijamii na kiuchumi kupitia tafiti za kisayansi, elimu na utungaji na utekelezaji wa sera mbalimbali.



## Benki ya Dunia yatoa wito wa kuharakisha utekelezaji wa shughuli za Mradi wa HEET huku UDSM ikionyesha maendeleo ya kupigiwa mfano

*Inatoka Uk. 21*

### *Maendeleo ya Kutiliwa Mfano UDSM*



*Kiongozi Mkuu wa Kimataifa wa Elimu ya Juu katika Benki ya Dunia ambaye pia ni Kiongozi wa Timu ya Utekelezaji Bi. Roberta Malee Bassett.*

Dkt. Liberato Haule, Naibu Mkurugenzi wa Mradi wa HEET-UDSM, alieleza maendeleo ya mradi ambayo yanaonekana kutia moyo kwani yako ndani ya muda wa utekelezaji. Alieleza kuhusu ujenzi unaoendelea wa majengo mapya katika maeneo ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ya Lindi na Kagera, pamoja na ujenzi wa majengo huko Buyu, Zanzibar kwa ajili ya Taasisi ya Sayansi za Baharin alisema:

"Miradi yote imepangwa kukamilika mapema mwaka 2026, na uongozi wa UDSM umejizatiti kuhakikisha inakamilika ndani ya muda uliopangwa licha ya changamoto zilizopo," alisema Dkt. Haule.

Pia, alibainisha miradi muhimu katika Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere Mlimani, Dar es Salaam, ikiwamo ujenzi wa Kituo cha Jinsia na Watu Wenye Mahitaji Maalum.

"Kituo hiki kinajengwa kwa lengo la kutoa huduma muhimu kama vile unasihi, upatikanaji wa rasilimali za kitaaluma, na programu maalum za msaada kwa makundi yanayoathiriwa na masuala ya kijinsia na wanafunzi wenye ulemavu," alieleza.

Dkt. Haule alisisitiza kuwa kituo hicho kitakuwa na jukumu muhimu katika kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wanapata mahitaji muhimu kwa ustawi wao kitaaluma.

Mradi mwingine mkubwa unaoendelea ni ujenzi wa hosteli ya kisasa ya wanafunzi wa shahada za uzamili jijini Dar es Salaam, ambayo inatarajiwa kukidhi mahitaji yanayoongezeka kila uchao ya malazi ya kiwango cha juu kwenye kampasi.

"Mradi huu utajengwa kisasa na kutoa mazingira wezeshi ya kuishi ili kuunga mkono jitihada za kitaaluma za wanafunzi wa shahada za uzamili," alisema Dkt. Haule.

UDSM inajenga majengo 24 chini ya Mradi wa HEET kwa ajili ya shughuli za kitaaluma na kiutawala, ikiwamo majengo katika Taasisi ya Sayansi za Baharini (IMS) iliyopo Buyu, Zanzibar, na kampasi mpya katika mikoa ya Kagera na Lindi.

Mradi huu unaofadhiliwa na Benki ya Dunia, ni matokeo ya jitihada za ulinganishi viwango unaolenga kubadilisha elimu ya juu nchini Tanzania kwa kuboresha miundombinu, kupitia mitaala na kuimarisha uwezo wa kitaasisi katika taasisi za elimu ya juu nchi nzima.

## Waziri Jafo asisitiza ubiasharishaji wa matokeo ya utafiti na kuzingatia ustawi wa jamii

*Inatoka Uk. 20*

### *Nafasi ya utafiti na ubunifu katika ustawi wa jamii*

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Prof. William A.L. Anangisye, alisisitiza dhamira ya chuo ya kuunganisha utafiti na mahitaji halisi ya jamii chini ya Dira ya UDSM ya mwaka 2061. "Warsha hii imedhihirisha dhamira yetu ya kuhakikisha ubora wa utafiti unachochea mageuzi ya kijamii," alibainisha.

Prof. Anangisye alitaja baadhi ya jitihada muhimu kama vile Kituo cha Ubiasharishaji Utafiti, Wiki ya Utafiti na Ubunifu ambayo hufanyika kila mwaka, pamoja na programu za kujenga uwezo katika masuala ya milikihidhini. Hata hivyo, alikiri kuwa kasi ya ubiasharishaji wa matokeo ya kazi za utafiti bado inahitaji kuongezwa.

Prof. Nelson Boniface, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo – Utafiti, alisisitiza mwelekeo mpya wa ubunifu unaoilenga jamii, akitangaza mpango wa kuanzisha taasisi mpya itakayolenga ustawi wa jamii amesema: "Taassisi hii itakuwa nguzo ya jitihada shirikishi za sekta mbalimbali katika kukabiliana na changamoto zinazoikabili jamii kama vile umaskini, afya na uhimilivu wa mazingira".

### *Maonesho, midahalo na ushawishi wa sera*

Warsha iliyofanyika chini ya Mradi wa HEET, iliwiana na Mpango Mkakati wa Miaka Mitano wa UDSM na iliwakutanisha pamoja watafiti, wabunifu, wawakilishi wa serikali, sekta binafsi, benki na washirika wa maendeleo.

Warsha ilishirikisha bunifu 37 za kisasa ikiwa ni pamoja na teknolojia ya kilimo na masuluhisho yanayotolewa na akiliunde zilizoonyeshwa na wanafunzi na wafanyakazi wa UDSM. Siku ya mwisho ilijumuisha majadiliano ya kimkakati kuhusu sera, majadiliano ya kujenga mtandao na ushirika, vyote vikilenga kujumuisha ubunifu katika ajenda za taifa za viwanda na maendeleo jumuishi.

Kadri Tanzania inavyoelekea katika uchumi unaotegemea maarifa chini ya Dira ya 2050, uongozi wa UDSM unatarajiwa kuhamasisha maendeleo endelevu na mageuzi ya kijamii kote nchini kupitia mpango wa ubiasharishaji wa matokeo ya kazi zinazotokana na matokeo ya utafiti

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

HEET
HIGHER EDUCATION FOR ECONOMIC TRANSFORMATION


## Mawasiliano

Naibu Mratibu: +255 765 939 958

Mhariri Mkuu: +255 755 172 570

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam,
Jengo la Cranford Pratt,
Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere, Mlimani
Barabara ya Chuo Kikuu, 16103 Ubungo
S.L.P. 35091
Dar es Salaam, Tanzania

heet@udsm.ac.tz Heet Udsm www.udsm.ac.tz